TANGAZO LA SERIKALI NA. 77 la tarehe 7/2/2025

SHERIA YA BODI YA UTALII TANZANIA,
(SURA 364)

# KANUNI

*(Zimetengenezwa chini ya kifungu cha 14)*

KANUNI ZA MABALOZI WA HIARI WA UTALII, 2025

## MPANGILIO WA KANUNI

*Kanuni* *Jina*

SEHEMU YA KWANZA
MASHARTI YA UTANGULIZI

1. Jina.
2. Tafsiri.

SEHEMU YA PILI
UTEUZI WA MABALOZI WA HIARI WA UTALII

3. Sifa za uteuzi.
4. Maombi.
5. Uchakataji wa maombi.
6. Mapendekezo ya uteuzi.
7. Uteuzi wa balozi wa hiari wa utalii.
8. Muda wa kuhudumu.
9. Majukumu ya balozi wa hiari wa utalii.
10. Masharti ya balozi wa hiari wa utalii.
11. Kutengua uteuzi.

SEHEMU YA TATU
MASHARTI MENGINEYO

12. Rejista ya mabalozi wa hiari wa utalii.
13. Kutambuliwa kwa balozi wa hiari wa utalii.
14. Adhabu.

---

MAJEDWALI

---

SHERIA YA BODI YA UTALII TANZANIA,
(SURA 364)

---

KANUNI

---

*(Zimetengenezwa chini ya kifungu cha 14)*

KANUNI ZA MABALOZI WA HIARI WA UTALII, 2025

SEHEMU YA KWANZA
MASHARTI YA UTANGULIZI

Jina

1. Kanuni hizi zitajulikana kama Kanuni za Mabalozi wa Hiari wa Utalii za mwaka 2025.

Tafsiri

2. Katika Kanuni hizi, isipokuwa kama muktadha utahitaji vinginevyo:

Sura ya 364

"balozi wa hiari wa utalii" maana yake ni mtu mashuhuri, mwenye kipaji na ushawishi ambaye ameridhia kujitolea muda wake, kipaji na mapenzi ya kuitangaza Tanzania kama kivutio cha utalii kinachopendelewa zaidi ndani na nje ya Tanzania;

"Bodi" maana yake ni Bodi ya Utalii Tanzania iliyoanzishwa chini ya kifungu cha 3 cha Sheria;

"Mkurugenzi Mtendaji" maana yake ni Mtendaji Mkuu wa Bodi ya Utalii Tanzania aliyeteuliwa chini ya kifungu cha 6 cha Sheria;

"mtalii" maana yake ni mtu ambaye anasafiri kwenda sehemu nje ya eneo lake la makazi ya kawaida kwa muda kati ya saa ishirini na nne na mwaka mmoja na

madhumuni ya safari yake ni tofauti na utekelezaji wa shughuli inayompatia kipato kutoka ndani ya sehemu aliyotembelea:

Isipokuwa kwamba, iwapo shughuli inatekelezwa na mkazi wa Tanzania, mtu huyo atajulikana kama mtalii wa ndani;

"Sheria" maana yake ni Sheria ya Bodi ya Utalii Tanzania;

"Waziri" maana yake ni Waziri mwenye dhamana ya masuala ya utalii; na

"Wizara" maana yake ni Wizara yenye dhamana ya masuala ya utalii.

## SEHEMU YA PILI
## UTEUZI WA BALOZI WA HIARI WA UTALII

Sifa za uteuzi

3. Mtu anaweza kufikiriwa kwa ajili ya uteuzi kama balozi wa hiari wa utalii ikiwa atakuwa na sifa zifuatazo:

(a) ana sifa njema na mwenendo mzuri katika jamii;
(b) ni mtu mashuhuri na mwenye utayari wa kutangaza malengo ya utalii wa Tanzania kwa hiari;
(c) ana mtandao mpana wa kijamii;
(d) ana uwezo wa kushawishi na kutangaza mazao ya utalii, mikakati na shuguli za kitalii za Tanzania; na
(e) hana historia ya kutenda kosa la jinai.

Maombi

4.-(1) Mtu ambaye anakusudia kuteuliwa kuwa balozi wa hiari wa utalii atawasilisha maombi kwa Mkurugenzi Mtendaji katika namna iliyoainishwa kwenye Fomu Na. 1 iliyoainishwa katika Jedwali la Kanuni hizi.

(2) Fomu ya maombi iliyojazwa itaambatana na-

(a) kitambulisho cha Taifa;
(b) cheti cha taaluma katika masuala ya utalii, ikiwa anacho; na
(c) barua ya mapendekezo kutoka kwa taasisi au kampuni ya utalii inayotambuliwa na Bodi.

Uchakataji wa maombi

5.-(1) Mkurugenzi Mtendaji, baada ya kupokea maombi chini ya Kanuni hizi, atafanya upekuzi juu ya sifa za mwombaji.

(2) Upekuzi chini ya kanuni ndogo ya (1) utakuwa kwa madhumuni ya-

(a) kujiridhisha na uzoefu wa mwombaji ili kuhakikisha kuwa ana sifa na utaalamu utakaomwezesha kutekeleza majukumu yake chini ya Kanuni hizi;

(b) kubainisha utayari wa mwombaji kujitolea kutangaza utalii; na

(c) kubainisha masuala mengine yeyote muhimu.

(3) Mkurugenzi Mtendaji baada ya kufanya upekuzi juu ya sifa za mwombaji, na baada ya kuridhika ipasavyo, atawasilisha taarifa na mapendekezo yake kwa Bodi kwa ajili ya ridhaa.

(4) Endapo Mkurugenzi Mtendaji hataridhika na maombi, atamtaarifu mwombaji ndani ya siku thelathini na kumpa sababu za kutoridhika.

Mapendekezo ya uteuzi

6. Bodi, baada ya kupokea taarifa na mapendekezo kwa mujibu wa kanuni ya 5, Bodi itafanya mapitio ya maombi na kufanya uamuzi wa kuridhia maombi au kukataa maombi kumjulisha mwombaji sababu za kukataliwa kwa maombi.

Uteuzi wa balozi wa hiari wa utalii

7.-(1) Bodi baada ya kuridhia maombi chini ya kanuni ya 6, itawasilisha jina la mwombaji kwa Waziri kwa ajili ya kuidhinishwa.

(2) Waziri baada ya kumuidhinisha mwombaji atamteua mtu aliyependekezwa kuwa balozi wa hiari wa utalii na kutoa cheti kwenye Fomu Na. 2 kama ilivyoainishwa katika Jedwali la Kanuni hizi.

(3) Bila kujali masharti ya kuwasilisha maombi ya kuteuliwa kuwa balozi wa hiari wa utalii, Waziri anaweza, kwa kushauriana na Bodi, kumteua mtu yeyote mwenye sifa zilizoainishwa chini ya Kanuni hizi kuwa balozi wa hiari wa utalii.

Muda wa kuhudumu

8. Balozi wa hiari wa utalii atahudumu kwa muda wa miaka miwili kuanzia tarehe ya uteuzi na anaweza kuteuliwa tena.

Majukumu ya balozi wa hiari wa utalii

9. Balozi wa hiari wa utalii atakuwa na wajibu na majukumu yafuatayo:

(a) kuhamasisha watalii na wawekezaji kutembelea au

kuwekeza nchini Tanzania;
(b) kuhamasisha uhifadhi wa rasilimali asilia, za kiutamaduni na za kihistoria;
(c) kuitangaza Tanzania kama kituo kinachoongoza katika vivutio vya utalii duniani;
(d) kulinda taswira ya nchi katika masuala ya utalii.

Katazo

10. Mtu aliyeteuliwa kuwa balozi wa hiari wa utalii hatatakiwa, katika utekelezaji wa wajibu na majukumu yake:
(a) kujihusisha na vitendo vyovyote vya ubaguzi;
(b) kujihusisha na vitendo au matukio yanayosababisha uvunjifu wa amani au uhalifu wa aina yoyote;
(c) kujihusisha katika vitendo vinavyochafua taswira ya sekta ya utalii;
(d) kujihusisha na vitendo vya udanganyifu, utapeli au upotoshaji;
(e) kutumia taarifa na nyenzo za utangazaji alizopata katika utekelezaji wa wajibu na majukumu yake kwa manufaa binafsi; na
(f) kujihusisha na biashara ya utalii au shughuli zinazoweza kusababisha mgongano wowote wa maslahi.

Kutenguliwa kwa uteuzi

11. Waziri anaweza kutengua uteuzi wa balozi wa hiari wa utalii endapo:
(a) atashindwa kutekeleza majukumu yake kama ilivyoainishwa katika Kanuni hizi;
(b) atapoteza sifa za kuteuliwa kuwa balozi wa hiari wa utalii zilizoainishwa katika Kanuni hizi;
(c) atakuwa na mwenendo unaochafua taswira ya sekta ya utalii Tanzania;
(d) atatiwa hatiani kwa kosa la jinai;
(e) atashindwa kuzingatia masharti yaliyoanishwa katika kanuni ya 10; na
(f) kuna jambo linalohusu maslahi ya umma.

## SEHEMU YA TATU
## MASHARTI MENGINEYO

*Tangazo la Serikali Na. 77 (Linaendelea)*

Rejesta ya mabalozi wa hiari wa utalii

12.-(1) Bodi itaandaa na kutunza rejesta ya mabalozi wa hiari wa utalii.

(2) Rejesta iliyoandaliwa chini ya kanuni ndogo (1) itakuwa na maelezo ya mabalozi wa hiari wa utalii.

Kutambuliwa kwa mabalozi wa hiari wa utalii

13. Balozi wa hiari wa utalii aliyeteuliwa chini ya Kanuni hizi-

(a) atatambuliwa na Wizara, Balozi za Tanzania nje ya nchi na wadau wa utalii ambao watatakiwa kumpa ushirikiano katika kutekeleza majukumu yake;

(b) anaweza kupewa taarifa na nyenzo za utangazaji kwa ajili ya kutekeleza majukumu yake kwa ufanisi;

(c) anaweza kunufaika na motisha za safari zinazoandaliwa na Bodi na wadau wengine wanaotambulika kwenye maeneo yenye vivutio kwa ajili ya kujijengea uelewa.

Adhabu

14. Mtu yeyote atakayejitangaza kuwa balozi wa hiari wa utalii bila kuteuliwa kwa mujibu wa Kanuni hizi atakuwa ametenda kosa na akitiwa hatiani atawajibika kulipa faini ya kiasi kisichozidi shilingi laki sita au kifungo kisichopungua miezi sita na kisichozidi miezi kumi na mbili.

*Tangazo la Serikali Na. 77 (Linaendelea)*

JEDWALI

*(Imetengenezwa chini ya kanuni 4(1) na 7(2))*

TTB Fomu Na. 1

FOMU YA MAOMBI YA UTEUZI WA BALOZI WA HIARI WA UTALII

Mimi ……………………………………. wa anuani. …………..….. ninaomba kuteuliwa kuwa balozi wa hiari wa utalii.

Nina sifa za kuweza kuteuliwa kuwa balozi wa hiari wa utalii kama ifuatavyo:………………………………………………………………………………
………………………………………………………………………………………………
…………………………………………………
………………………………………………………………………………………………
……………………….
………………………………………………………………………………………………
………………………
Wadhamini wangu ni:
…………………………………………………..
………………………………………………….
………………………………………………….

Ninaahidi kufuata masharti yote yanayohusiana na utendaji wa balozi wa hiari wa utalii.

…………………………………..
………………………
Tarehe Saini
ya mwombaji

*Tangazo la Serikali Na. 77 (Linaendelea)*

TTB Fomu Na.2

CHETI CHA UTEUZI WA BALOZI WA HIARI WA UTALII

Na. …………..

HII ni kuthibitisha kuwa …………………. Ameteuliwa kuwa Balozi wa Hiari wa Utalii.

Imetolewa leo tarehe ……..…. mwezi………………… 20………..

| | | |
|---|---|---|
| ………………….. | ………………… | ………… |
| Tarehe | Jina | Saini |
| | | *Waziri wa Maliasili na Utalii* |

Dodoma
3 Februari, 2025

PINDI HAZARA CHANA,
*Waziri wa Maliasili na Utalii*